

# UQAB
Jarida la

*Toleo 23 - Rabi-ul-Awwal 1440 H / Disemba 2018 Miladi*

**Rabiul-Awwal: Mwezi wa Upambanuo Baina ya Batili na Haki**

**Urusi ni Mbwa Mwitu Aliyejivika Ngozi ya Kondoo!**

**Maana ya Shahada Laa ilaha ila Llah**

**Athari ya Kuvunjika kwa Familia Juu ya Watoto na Jamii**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 18**

**SWALI/JAWABU: Msisitizo wa Trump Juu ya OPEC**



## Yemen: Maswali ambayo kila mmoja anatakiwa kujiuliza!

# Yemen: Maswali ambayo kila mmoja anatakiwa kujiuliza!

Inawezekana vipi kujiandaa kila siku tukiwa na akili timamu, kuwaandalia chakula kizuri watoto wetu, kuwavisha mavazi mazuri na masafi na kuwalea kwa utulivu na mapenzi tukiwalaza, **LAKINI tukitazama kiuzembe** takribani watoto milioni 1.8 wa Ummah huu ndani ya Yemen wakidhoofika na kuangamizwa bila huruma? Inawezekana vipi sisi tuwe na furaha kwamba watoto wetu wanakuwa na kustawi, wakati takribani watoto 500,000 ndani ya Yemen hawataona siku ya kuzaliwa kwao kutokana na vita vya leo dhidi ya Uislamu?

Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani zimshukie, alisema:
«مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادِّهِمْ، وَتَرَاحُمِهِمْ، وَتَعَاطُفِهِمْ مَثَلُ الْجَسَدِ إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالسَّهَرِ وَالْحُمَّى»
“Maajabu ya waumini katika kupendana kwao, kuhurumiana kwao ni kama mwili mmoja. Wakati kiungo kimoja kinaumwa, mwili mzima unashughulishwa kwa kuupelekea kuwa na homa na kukosa usingizi.” (Sahih al Bukhari)

Haituumi kuona kuwa Ummah wa Waislamu uko katika hali hii mbaya leo? Hatuna mioyo myepesi ya kuhisi machungu haya ya kutisha wanayopitia kaka zetu, dada zetu na watoto wetu Waislamu? Je dunia yenye kuhadaa imetutia upofu kiasi kwamba tumezama ndani ya maisha yetu na matatizo yetu madogo tukisahau kuwa Ummah upo ndani ya mvutano hivi sasa na kwamba mtoto mdogo Muislamu asiyekuwa na makosa anaota kuhusu kipande cha mkate? Hakika tukijitia hamnazo juu ya uhalifu huu; basi hakutakuweko na khair yoyote ndani ya mioyo yetu!
Mtume (saw) alisema:
«إِنَّ فِي الْجَسَدِ مُضْغَةً إِذَا صَلُحَتْ صَلُحَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، وَإِذَا فَسَدَتْ فَسَدَ الْجَسَدُ أَلَا وَهِيَ الْقَلْبُ»
“Kuna kijinyama ndani ya mwili- kikiwa kizuri, mwili mzima umekuwa mzuri. Kikiwa kibaya, mwili mzima umekuwa mbaya. Hakika ni moyo huo.” (Sahih al Bukhari)

Hisia juu ya Ummah ni hisia muhimu. Habari kuhusu hali ya Ummah ni ufahamu muhimu. Lakini hisia na ufahamu pekee hazitoshi kuuondosha uchungu wa Ummah. Ni vyanzo na msingi ambao hukamilika pale tunapotia hisia na fikra zetu na kuzifanyia kazi!

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عِلْمٍ لَا يَنْفَعُ، وَمِنْ قَلْبٍ لَا يَخْشَعُ، وَمِنْ نَفْسٍ لَا تَشْبَعُ، وَمِنْ دَعْوَةٍ لَا يُسْتَجَابُ لَهَا»
“Ewe Mwenyezi Mungu, naomba msaada Wako unilinde kutokana na elimu isiyo na manufaa, kutokana na moyo usiokuwa na hofu juu ya Mwenyezi Mungu, kutokana na nafsi isiyotosheka na kutokana na dua ambayo haikujibiwa.” (Sahih Muslim)

Tunaona wazi kuwa maadui wa Uislamu hawatousaidia Ummah na kuwaletea kuwa kitu kimoja. Watawasababishia ugomvi zaidi baina yao na kuwapatiliza wao na nchi zao ili kufikia mipango yao miovu.

Na iko wazi kuwa ni kupitia kubadilishwa kwa uongozi wa kiulimwengu, ambao pekee Khilafah kwa njia ya Utume itaweza kubadilisha hali ya Waislamu. Kwa sababu ni kiongozi ambaye ni mchaMungu, yuko makini kuhakikisha Ummah wake haulali njaa na anaulinda dhidi ya maangamivu yoyote.

Kwa nini watu wengi bado wanaamini kuwa Marekani au Ufaransa ndiyo wanao wajali na kuwasaidia Waslamu???

Kwa sababu ni njia ya wazi, inayowadanganya Waislamu na kuwafanya mioyo yao idunde sio kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu bali kwa ajili ya dunia. Ni njia ambayo inawatia motisha Waislamu ili wasione kwamba nguvu kubwa za ulimwengu ndiyo adui mkubwa wa Uislamu. Hatimaye ndiyo njia ya kuugawanya Ummah na kuifanya mioyo yao kuwa migumu na kuwatia upofu.

**Kaka na Dada Wapendwa!**
Uamuzi tunao mikononi mwetu kuhusu ni njia gani ya kufuata! Ima sisi ni Waislamu tunaowafanya marafiki maadui wa Uislamu. Au sisi ni Waislamu tunaojali tu kuhusu mambo yetu ya kidunia au sisi ni Waislamu tunaojipa matumaini kupitia michango midogo au sisi ni Waislamu tunaofanya kazi usiku na mchana kuhakikisha tunaleta ukombozi wa kweli wa Ummah kupitia kazi ya kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume.
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ
“Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu.” [Muhammad: 7]


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Amanah Abed**





Email: info@uqab.or.ke

# Rabiul-Awwal: Mwezi wa Upambanuo Baina ya Batili na Haki




Ummah wa Kiislamu ulimwenguni kote upo katika harakati za kusherehekea kuzaliwa kwa Bwana na Kipenzi chetu Muhammada ibn Abdullah (saw). Ni mwezi uliojaa nishati na furaha kwa Ummah wa Kiislamu duniani. Kila mwanachama wa Ummha huu mtukufu daima hapitwi na tukio hili adhimu ambalo ni msingi madhubuti wa mwamko wa Ummah huu. Kwani (saw) alikuwa ni Mtume wa mwisho kuwahi kutumwa ulimwenguni.

رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ

"(Muhammad) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii." [Al-Ahzaab: 40]

Na ujumbe wake ni kwa walimwengu wote kinyume na mitume waliotangulia:

وَمَآ أَرْسَلْنَـٰكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَـٰلَمِينَ

"Nasi hatukukutuma (Muhammad) ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote." [Al-Anbiyaa: 107]

Na hakika kuja kwake ni Nuru iliyoangaza juu ya ulimwengu na kitabu alichopewa kinabainisha baina ya Haki na Batili:

قَدْ جَآءَكُم مِّنَ ٱللَّهِ نُورٌ وَكِتَـٰبٌ مُّبِينٌ

"Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru (Muhammad) na Kitabu (Qur'an) kinacho bainisha (Haki na Batili)." [Al-Maaida: 15]

Kwa masikitiko makubwa Mwezi huu umetujia lakini Waislamu tumo katika hali duni na tuliojawa na hizaya kutoka kila pembe. Hali hii imetokana na Ummah huu mtukufu wa Kiislamu kujiweka mbali na mafundisho ya Nuru (Muhammad) na Kitabu (Qur'an). Badala yake umejisalimisha kutawaliwa na mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali unaotokana na dola za kimagharibi za kikoloni. Dola hizi za kimagharibi ndizo zilizosambaza sumu kupitia itikadi yake ya kiilmaniyah (kutenganisha dini na maisha). Itikadi hii ndiyo chanzo kilichowapelekea baadhi ya wanachama wa Ummah huu mtukufu wa Kiislamu kusalitika nayo na kuwapelekea kufanyakazi na kushirikiana na viongozi wa kimagharibi katika Kumdunga Kisu Mama wa Faradhi zote Katika Uislamu – Khilafah. Kisha wakaivunja na kuigawa vipande vipande na kukabidhiwa kama ngawira kwa wajinga wakubwa wakiongozwa na Mustafa Kamal aliyepewa Uturuki iliyokuwa ndiyo makao makuu ya Khilafah kabla kuiangusha. Akifuatiwa na Sharrif Hussein na wanawe wakipewa Saudi Arabia, Iraq na Jordan n.k.

Endelea Uk..4

Kuangushwa kwa Dola ya Kiislamu ya Khilafah ndiyo chanzo cha hizaya juu ya Ummah huu mtukufu ambao kitakwimu unakaribia bilioni 2! Licha ya kuwa Ardhi za Waislamu ndiyo chanzo cha rasilimali muhimu zenye kuendesha uchumi wa dunia kwa mfano mafuta, gesi na madini n.k bado wafuasi wake wanazama ndani ya umasikini wa kupindukia kuanzia Yemen, Somalia, Iraq n.k. Majeshi yake lau yataunganishwa chini ya Dola moja basi litakuwa jeshi kubwa duniani na lenye zana nyingi! Tukichukua rasilimali, majeshi na Waislamu wote duniani chini ya Dola Moja ya Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume inayoongozwa na Khalifah mchaMungu anayetawala kwa Qur'an na Sunnah; kattu hakuna atakayejaribu kuwacheza shere Waislamu na kuzimwaga damu zao kama inavyoshuhidwa hjvi leo nchini Palestina, Somalia, China, Afghanistan, Kashmir, Syria n.k. Hakika kama alivyofanya Mtume (saw) juu ya Kabila la Kiyahudi la Banu Qaynuqa lililomchezea shere mwanamke mmoja Muislamu likafurushwa kabila lote! Nalo Kabila la Kiyahudi la Banu Qurayza lililowaendea kinyume Waislamu, wanaume wao wote waliobaleghe wakauliwa! Na mifano mingi chini ya Makhalifa wachaMungu kuanzia Abu Bakar (ra) mpaka Khalifa wa mwisho Abdulhamid wa Pili; hakuna aliyejaribu kuwaotesha kidole Waislamu au Uislamu wao.

Lakini hivi leo Uislamu hautawali hakuna ngao ya Waislamu ili kuwaunganisha Waislamu chini ya twaa ya kiongozi mmoja. Kinyume chake kila mmoja amebakia kujifunga na utaifa wake kwa mujibu wa mipaka iliyochorwa na wakoloni wamagharibi na kuzama ndani ya hisia za kizalendo kiasi kwamba Muislamu aliyeko Tanzania/Pakistan/Libya/Syria anamuona wa Kenya/CAR/Afghanistan/Palestina ni mgeni na kamwe hana ukuruba naye; na matatizo yake ni yake wala hayamuhusu! Ilhali Ummah huu ni Ummah Mmoja sawa na Mwili Mmoja:

**"Waumini katika kuhurumiana kwao ni kama mwili mmoja. Wakati kiungo kimoja kinaumwa, mwili mzima unashughulishwa kwa kuupelekea kuwa na homa na kukosa usingizi."** [Bukhari na Muslim]

Kwa hivyo hatuna budi kuitikia Mwito wa Kurudisha Maisha ya Kiislamu kupitia kurudisha tena serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Hakika kupitia kufanya kazi hii ndiko kunakopelekea mwanadamu kupata ladha ya maisha na utulivu wa nafsi. Kwani ni kupitia kurudi kwa Khilafah ndiko kutakako hakikisha kunaondosha udhalimu na maonevu wanayopitia Waislamu na wasiokuwa Waislamu ulimwenguni chini ya mikono na sera fisadi za wamagharibi wakoloni kutokana na mfumo wao wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake angamivu ikiwemo demokrasia n.k.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱسْتَجِيبُوا۟ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

"Enyio mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele." [Al-Anfaal: 24]

Ni jukumu letu Waislamu wote hususan viongozi katika Ummah wapatilize msimu huu na kuwatangazia Waislamu Uyatima waliokuwa nao na Ufaradhi wa Kurudisha Khilafah ili kuuondosha uyatima huo! Ama kwa walio na nguvu miongoni mwa majeshi katika watoto Mukhlisina Waislamu ndani ya nchi za Waislamu mfano Pakistan, Misr, Iraq, Jordan n.k waitiekie mwito huu kwa kutoa Nusrah na wajue kuwa malipo yao ni Pepo kama vile walivyoahidiwa Khaws na Khazraj (Ansar) wachangamke na kwa hakika wataingia katika historia kama alivyoingia katika historia Sa'd ibn Mu'adh (ra) kutokana na dori kubwa aliyocheza katika kuunusuru Uislamu na Waislamu na ikapelekea:

**"Kiti cha enzi ya Mwenyezi Mungu kimetikisika kutokana na kifo cha Sa'd ibn Mu'adh."** [Bukhari na Muslim]

Hitimisho; kila anayesheherekea kuzaliwa kwa Mtume (saw); ajiulize **"Je Qur'an na Sunnah ndiyo Muongozo/ Mfumo wetu Katika Maisha Jumla (Kisiasa, Kijamii, Kiuchumi, Kielimu n.k)?** Na awe mkweli katika jibu lake na ajue kuwa atakwenda kuulizwa Siku ya Kiyama mbele ya Mwenyezi Mungu "**Je ulicheza dori gani wakati Qur'an na Sunnah zilikuwa SIO Muongozo Katika Maisha Jumla?"** Wakati ni sasa kujiunga na kufanyakazi katika safu iliyobeba kheri kubwa kuliko kheri zote nayo ni safu ya Ulinganizi wa Kurudi tena Khilafah kwa Njia ya Utume. Safu isiyopaka mtu mafuta wala kupinda aya kwa ajili ya maslahi au kuogopa vitisho vya wanaotishia! Bali daima kila siku safu hii inaelekea kufikia bandarini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kwani Yeye ndiye huumpa Ushindi Amtakaye.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Urusi ni Mbwa Mwitu Aliyejivika Ngozi ya Kondoo!




Tarehe 22 Oktoba 2018 kulifanyika Kongamano la Kwanza la Kijamii kati ya Urusi na Afrika (Russian-African Social Forum) lililoandaliwa na Muungano wa Dunia wa Masuala ya Kigeni ya Vyuo Vikuu vya Urusi na Afrika na Muungano wa Mipango ya Kibiashara ya Afrika, lilifanyika Moscow. Zaidi ya watu 500 walishiriki: watu maarufu kutoka Urusi na Afrika katika siasa na umma, wawakilishi wa kitaaluma, jamii ya wafanyibiashara na wawakilishi wa mashirika ya wanafunzi na vijana. Tukio hilo lilitoa nafasi maalum ya kubadilishana mawazo juu ya masuala ya kisasa kuhusiana na mahusiano kati ya Urusi na nchi za Afrika, hali ya sasa ya mahusiano na uwezekano wa kuzidisha maendeleo katika nyanja za kisiasa, kibiashara, kiuchumi, ubinadamu, vitengo vya kitamaduni pamoja na mengineyo. (Eurasia Review, 30/10/2018)

Mkutano huu umezidi kubainisha 'usanii' wa elimu ya kibepari na uhalisia wa 'msaada/udhamini' wa kielimu. Kwa kuwa washiriki wengi walikuwa ni wahitimu wa vyuo vya Urusi kwa miaka tofauti kutoka nchi mbalimbali, bila shaka wengi ni kutoka Afrika inaonesha namna ulivyo mfumo wa elimu duniani na natija ya ufadhili wa masomo.

Waziri wa Kigeni Sergey Lavrov alisema yafuatayo katika kauli yake ya ufunguzi wa Kongamano la Kijamii kati ya Urusi na Afrika: **"Nchi yetu haikujipaka tope ya uhalifu wa ukoloni. Kinyume chake, ni kwamba ili wasaidia kwa kila hali, watu wa bara la Afrika katika kupata uhuru na ubwana wao kwa kuwapa misaada ya kuendelea na usaidizi katika kujenga mataifa yao na kumakinisha uhuru wa kiuchumi wa mataiafa ya Afrika. Tunajivunia kufaulu katika ushirikiano wa kisiasa, kiuchumi, kimatamaduni na nyanga ningenezo." (The Ministry of Foreign Affairs of the Russian Federation, 22/10/2018)**

Nchi zilizoendelea hutumia nafasi ya 'ufadhili' wa kimasomo ili kuwapa thaqafa (fikra) na kuwaandaa wanafunzi hao kuwa visemeo vyao pindi warudipo makwao ili wasifie na kujivunia nchi wafadhili kwa kila chao na kushawishi ifunguliwe milango kwa ajili ya nchi wafadhili 'kuwekeza' na kujenga athari, kisha nao (wanafunzi) lau wakipata uongozi kuwa wakala wa wafadhili wao wa kielimu, imma kwa kudhamiria au kutodhamiria, kwa sababu akili zao ndivyo zilivyojengwa. Ndiyo 'wasomi' hao ambao la kwanza katika kubadilika kwao 'kisomi' ni kuiga tamaduni za nje na kudharau za kwao, hata kama kimsingi za kwao ndiyo bora.

Utamaduni huu unaotokana na athari za ufadhili wa kielimu unagongana na kauli au dhamira ya kuwaacha waafrika kutatua matatizo yao wenyewe. Kwani elimu hufahamika kuwa ni nyenzo muhimu kwa mwanadamu, lakini siyo elimu hii ya kuwalisha wanafunzi thaqafa/

*Endelea Uk..6*

ustaarabu mgeni. Hatimaye wasomi hubakia kuwa wageni katika mazingira yao na hawaandaliwi kwa ajili ya kusaidia jamii zao kusonga mbele katika nyanja zote za maisha.
Kama alivyopata kunukuliwa Lord Macaulay, muasisi wa mikakati ya kielimu ya kimagharibi nchini India kwamba, "Ni lazima hivi sasa tufanye juhudi kubwa ili tujenge kikundi cha watu ambacho kitakuwa wafasiri wetu kati ya mamilioni tunaowatawala na sisi; kikundi cha watu ambao ni Wahindi kidamu na kirangi, lakini ni Wazungu kimtizamo, kimaoni, kimaadili na kiufahamu"

Ama kuhsu Urusi kuwa inaheshimu haki za binadamu tena za kidemokrasia halisi, hilo ni uwongo! Kihistoria katika zama za Ukomunisti, Urusi imesheheni historia ya kikatili na mauwaji ya mamilioni, kukandamiza dini, kudhulumu na kukandamiza raia kwa jumla. Na leo inaminya wapinzani wake, kuingilia masuala ya nchi jirani kama Ukraine, kuendelea na mauwaji ya kikatili ya wanawake, wazee na watoto nchini Syria bila ya kutaja dhulma na mateso wanayopata walinganiaji wa Uislamu nchini mwake wakiwemo walinganizi wa Hizb ut Tahrir waliobeba fikra angavu na kuukosoa mfumo batili wa kidemokrasia kwa njia ya fikra tu!

Ama kuhusu maendeleo ya Afrika, tatizo kubwa leo hii ni tatizo la kiaidiolojia/ kimfumo ambao hujenga na kuathiri mtazamo na mwendo wa mtu na taifa juu ya maisha. Urusi kwa sasa wamebaki kuwa wajamaa kinadharia tu, lakini ni mabepari katika mipango, mikakati na kimatendo. Matatizo yanayoikabili Afrika ndiyo hayo hayo kwa nchi zote duniani, ambayo ni kutokana na kutawaliwa na mfumo wa Ubepari.

Itawezekana vipi utatuzi huo wakati Urusi na madola mengine ya kibepari ya kikoloni wanapora usiku na mchana rasilimali za Afrika kama madini, kisha kuwaachia waafrika mashimo tu?! Aidha, itawezekana waafrika watatue matatizo yao ya Afrika ilhali wasomi wao ambao ndio tegemeo msingi na nyenzo muhimu katika juhudi hizo, wameshaharibiwa akili kwa kuandaliwa kinadharia zaidi, tena kwa manufaa ya wafadhili (Urusi)?!

Itawezekanaje kutatuka matatizo ya Afrika ilhali matatizo hayo na ya nchi nyengine changa ni mtaji na fursa kwa ustawi wa Urusi na nchi za kibepari jumla?! Kattu mataifa ya kimfumo wa kibepari hayapo na hayatakuwa tayari kuona 'makoloni' yao yakiimarika. Wameondoka kimwili lakini kimikakati bado wanakoloni. Viongozi wa nchi za Afrika ni vibaraka wao, wasomi ni visemeo vyao na wabeba agenda zao za maangamizi.

Ama kuhusu matamshi ya Waziri wa Kigeni wa Urusi kwamba Nchi yetu haikujipaka tope ya uhalifu wa ukoloni, ni dalili ya kibri na kuonesha wazi kwamba mkutano wao una lengo na ajenda ya kikoloni ili kuendeleza kupora rasilimali watu na vitu kwa ustawi wa nchi yao. Hawana lengo la utu, msaada, huruma wala mashirikiano ya dhati, zaidi ya muendelezo wa ukoloni mambo leo kwa sura ya kijanja. Sio ujamaa ulioanguka wala ubepari unaotawala leo hii ina uwezo wakutatua matatizo ya wanaadamu katika nchi yoyote. Mifumo hii ni tatizo mama na kamwe sio suluhisho, na yanayotangazwa kuwa ni matatizo ni matokeo na viashiria vya tatizo hilo.

Kwa leo, mfumo unaotawala wa kibepari kiasili unapuuza nafasi ya Mwenyezi Mungu Muumba, na badala yake unatukuza (kiumbe) akili ya binadamu kufikia kuiona kuwa inaweza kupangilia maisha yao kikamilifu na kwa usahihi kabisa. Pamoja na maendeleo yote ya kisayansi hayajawaongoza kuona na kukiri udhaifu wa mwanadamu kama kiumbe na kwamba hastahiki kujipangia namna ya kuishi bali anahitaji mjuzi zaidi ampangie na kumsimamia. Naye ni Mwenyezi Mungu.

Kupinga nafasi ya Mungu ndiko kunakoondoa utu katika nyoyo na mabongo ya binadamu na hatimaye kuzua vurugu na machafuko. Yakapatikana matabaka ya mabwana na watwana. Mabwana wakawa na maisha yao ya kuthamini zaidi mbwa wao, na kuacha binadamu wenzao (watwana). Watu wakauana ili kujiongezea mali (maslahi) kwani hilo ndiyo 'heshima' katika mfumo wa kibepari.

Suala kwa upana wake sio waafrika kwa Afrika yao, bali iwe walimwengu kwa Ulimwengu wao. Na utatuzi wa kweli na wa ufanisi haupatikani ila kwa kuondoa mfumo wa kibepari na kuweka mfumo mbadala, sahihi na kamili wa kuongoza maisha ya binadamu. Nao ni Uislamu pekee. Kama ulivyoshindwa ujamaa, na ubepari nao uko mahututi na unaendelea kuzalisha matatizo kila uchao.

Ni wakati sasa kuipa nafasi aidiolojia/ mfumo wa Kiislamu ili ustawishe jamii ya wanadamu bila ya kujali maeneo wala rangi zao. Na hili ni marudio tu, kwani historia inaushuhudia Uislamu kuwa ndio mfumo pekee bora uliowatawala wanadamu kwa muda mrefu na kwa mafanikio makubwa katika nyanja zote za maisha.

**Hamza Sheshe**
**Mwanachama wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Maana ya Shahada Laa ilaha ila Llah (لا إله إلا الله)




Tamko la(لا إله إلا الله) (Laa ilaha illa Allah) linalojulikana kama Shahada hutamkwa na Waislamu. Tamko linalojulikana pia kama tamko la Tawhid (upwekeshaji) ndio taklif ya kwanza kwa mtu yoyote yule atakaye kuingia kwa Uislamu. Kwenye Makala haya tutaliangalia tamko hili kwa kina zaidi ili tufahamu uzito wake na maana halisi yake. Pia ni muhimu kufahamu kuwa tamko hili la shahada ndiyo msingi wa Uislamu na msingi wa sheria zake yaani hukumu.

Tamko la shahada limeanza kwa herufi ya lam-alif (لا) ambapo hapa imebeba maana ya kukanusha jinsi zote (لا النافية للجنس) zile hivyo maana yake ni kusema hakuna/hapana. Laa sampuli hii huingia kwenye sentensi inayoanzishwa kwa jina. Kilugha ya Kiarabu sentensi hugawika mara mbili: Inayoanza kwa jina nayo huitwa (Jumla Ismiyyah) na nyengine ni inayoanza kwa kitendo (Jumla fiiliyyah). Kwa kuwa hapa imeingia kwenye sentensi ya kijina basi hubeba maana ya kutilia mkazo na kuthibitisha. Kwa hivyo hapa kuna msisitizo wa ukanushaji wa habari zinazofuata. Kwa maana hii inaposemwa 'laa ilaha' لا اله) (maana yake ni kukanusha kabisa kwa hakuna yeyote au chochote chenye kustahiki kuabudiwa. Kwa sehemu hii itakuwa ina maana watu wanapaswa kukanusha ibada kwa chochote kile na wala haimaanishi hakuna kuabudu kwa sababu ibada ni sehemu ya maumbile ya wanadamu. Ni maumbile ya kibinadamu kumtukuza Mungu hali inayomsukuma mwanadamu yeyote yule kuabudu chochote. Fauka ya haya kitarekh ya Mwanadamu hakukosekaniwa mahala pa kuabudu na cha kuabudiwa. Hiyyo ibada ni sifa/ishara ya kuweko na umbile kwa mwanadamu la kutukuza dini. Kwa maana haya ndiyo mwanadamu anapofanya ibada huwa ni mwenye kuhisi raha kwani katika huko kuabudu kwake atakuwa ameshibisha ile ghariza yake ya Kidini. Kuabudu kwa hali ya umaumbile hakufai kuachiwe kihamasa tu bali lazima kutumike akili pamoja na hisia ili kutambua nani apaswaye kupewa haki hii ya kumwabudu. Na hii ndiyo maana watu waliabudu viumbe kama vile majini, mawe, miti, watu na kadhalika.

Tukija kwa neno la اله (ilaha') ni jina la chochote/yeyote anayeabudiwa yaani waarabu huita chochote au yeyote mwenye kuabudiwa kwa jina hilo. Jina hili hapa lipo katika sifa ya umoja na pia maana yake ya kisheria na ya kilugha humaanisha maana moja tu nayo ni chochote / yeyote anayeabudiwa. Kwa muktadha huu, maana ya neno hili limefungika tu kwa maana moja ya kilugha na kisheria kwa tamko la Ilaha ni katika dalili kubwa na rehema ya Mwenyezi Mungu katika kusimamisha hoja kwa watu wote wasiamini mungu mwengine ila Mwenyezi Mungu pekee. Fauka ya haya Ilaha hapa sio lenya kuashiria jinsi maalum, aina hii ya jina huitwa nakira نكرة*) (jina ambalo halikufungika) nalo likitanguliwa na herufi ya 'laa' humaanisha hakuna ruhusa ya kuabudu chochote/yeyote. Hekima ya hilo ni kutaka kusiweko na mwenye kuabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu pekee. Na hapa ndiyo yaja uzito wa tamko hili la Tawhid.

Ama kuhusu ibara ya ila llah (الا الله); nayo ni kuwa hii ni ibara ya pili inayofuata na kutoa jibu la yule anayestahiki kuabudiwa. Kwenye lugha ya kiarabu herufi ya ILLA

Endelea Uk..8

hutumika katika kuvua jambo au kitu huku ikithibitisha baada ya kukanusha. Kwa maana itakua Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa aliye na haki ya kuabudiwa ni Mwenyezi Mungu pekee. Na haya ndiyo maelezo ya pili kwenye shahada yana mkalifisha mwenye kuitamka kutoabudu yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu. Kushuhudia kuwa Mwenyezi Mungu (swt) ndiye anayestahiki kuabudiwa kama inavyoelezwa kwenye shahada ni amri kwa Mwanadamu awe na Imani ya kihakika ya kumuamini Mwenyezi Mungu. Na kuwa yeyote asiyeamini hivyo anakuwa kafiri. Kama vilevile kutamka shahada kuna maanisha kuwa hakuna yeyote anayestahiki kuabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu nako pia ni amri ya kukanusha miungu.

Kupambika kwa Mwenyezi Mungu kuwa peke yake ndiye astahikiye kuabudiwa kwa haki kama ilivyo katika tamko hili la Tawhid ni kuelezwa kwa njia ya kukalifishwa na kutakikana watu wakubali na kusadikisha jambo hili tena pasina na shaka yoyote. Maelezo haya ni kutakikana kuitakidi msimamo huu ambao anayeitakidi kinyume chake au kupinga msimamo huu basi anakuwa kafiri. Aidha kuelezwa kuwa hakuna mungu mwengine ila Mwenyezi Mungu kama yalivyo maelezo ya shahada ni kutakikana kuamini mungu mmoja tu naye si mwengine ila Allah. Na yeyote atakayeamini uwepo wa mungu mwengine kinyume ya Allah basi ni kafiri vilevile.

**Aidha shahada inamaanisha yeyote anayeabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu ni urongo na batili:**

فَمَن يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِن بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

Basi anaye mkataa shetani (Kila chenye kuabudiwa kinyume na MwenyeziMungu) na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka yeye amekamata kishikio madhubuti kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. [Al-Baqara: 256]

Kufikia hapa ni kuwa kumwamini MwenyeziMungu sio kuwa ni kuamini tu kwamba yeye ni Muumbaji bali yeye ni mwenye kustahiki kufanyiwa ibada. Kwa maana haya shahada ya Laa ilaha illa LLah humaanisha hakuna yeyote anayestahiki kuabudiwa ila Allah. Hii ni kusema kwamba kalima hii inamwamrisha Muislamu kufungamanisha Imani yake moja kwa moja katika kumuabudu Mwenyezi Mungu (swt). Muislamu anaamrishwa kwa kutamka kalima hii kumtukuza Mwenyezi Mungu (swt) kwani Yeye ni muumbaji wa ulimwengu na vilivyomo ndani yake.

Katika ulimwengu wa kileo hasa ulimwengu wa Kimagharibi suala la kumwamini Mwenyezi Mungu (swt) huchukuliwa kuwa ni nidharia tu ambayo ukweli wake sio sana. Wanashikilia kwamba kuamini kuwepo kwa mungu ni fikra nzuri na husaidia mwanadamu kuepuka mabaya. Mtizamo huu ni hatari na kosa kubwa sana kwani masuala ya kumwamini Mwenyezi Mungu (swt) sio nadharia bali ni ukweli usokuwa na shaka.

Uislamu ukabainisha vizuri njia maalumu ya kumwamini Mwenyezi Mungu (swt) nayo ni kuwa Imani ya kuweko kwake ni ile inayotokamana na kukinai kwa akili na kutafakari utendakazi wake na Quran imebainisha wazi Imani ya kuweko kwa Allah (swt) Anayestahiki kuabudia. Asema Mwenyezi Mungu (swt):

وَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَٰنُ الرَّحِيمُ

“Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.”
[Al-Baqara: 163]

Kuelewa maana ya shahada ni jambo muhimu sana kwa Waislamu kwani haitakikani kwa mtu kushuhudia kitu asichokijua. Kwa bahati mbaya leo kutojua maana ya shahada ni moja wapo ya ujinga mkubwa sana licha ya wengi kuitamka shahada. Maisha yetu leo yako mbali mno na maana halisi ya shahada. Kwa hali hii Viongozi makhaini katika biladi za Kiislamu wanatawala maisha ya watu kwa kutegemea misingi ya Kisekula. Shahada leo imefungwa ndani ya Misikiti na kila anayejaribu kutanua maana yake hadi iongoze kwa maisha jumla basi hupachikwa jina kwa yeye ni mwenye misimamo mikali. Hivyo ni muhimu sana kufahamu maana halisi ya shahada yetu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# Athari ya Kuvunjika kwa Familia Juu ya Watoto na Jamii



Bwana Hakimu Coleridge, aliyekuwa hakimu wa familia nchini Uingereza akiwa na tajriba ya zaidi ya miaka 37 kuhusiana na sheria ya familia alilinganisha kuvunjika kwa maisha ya familia kuwa ni maangamivu sawa na athari ya mvuke wa kidunia. Alielezea kuwa ni tatizo linalo athiri nyanja zote za jamii na kwamba kila siku mahakimu kama yeye wanashuhudia “sherehe zisizoisha” za mahangaiko ya wanadamu, na kwamba “uovu wote wa jamii ukifuatiliwa unatokana na kuanguka kwa umadhubuti wa familia.” Bwana Coleridge hayuko pekee katika kuelezea athari za maangamivu ya kuvunjika kwa familia. Katika ripoti ya Kitengo cha Haki kwa Jamii (CSJ), ilionya kwamba Uingereza iko ndani ya “tsunami” ya kuvunjika kwa familia na athari mbaya juu ya watoto na jamii. Kuvunjika kwa maisha ya familia sio tatizo la kipekee kwa Uingereza bali ni tatizo la kiulimwengu, likitofautiana tu katika ukubwa ndani ya nchi tofauti. Tatizo linaonekana kuendelea kukuwa haraka ndani ya nchi ambazo maadili ya uhuru ya kimagharibi ndiyo yamepewa kipaombele. Kununukuu maneno ya mwanasiasa mkuu na mwenye tajriba wa Australia, Kevin Andrews, “Tishio kubwa linaloukumba ulimwengu wa kimagharibi sio mvuke wa kidunia, janga la kifedha au Uislamu wa misimamo mikali, bali ni kuendelea kuvunjika kwa miundo muhimu ya jamii ya umma –ndoa, familia na jamii.”

Vigezo kadhaa vinaweza kutajwa kama sababu ya kwa nini familia zinavunjika. Uzinifu, matatizo ya kifedha, vurugu, pombe na madawa ya kulevya ni baadhi tu ya sababu za kwa nini tunaona familia za vunjika. Matatizo yote haya yana athari mbaya kwa kila mtu ndani ya sehemu ya familia, lakini watoto ndiyo wahanga dhaifu wanaoathiriwa na kuvunjika kwa familia. Hii inatokana hususan kwa sababu ya kuwategemea wazazi ili kuwasaidia kukuwa watu wazima. Maisha ya familia katika kesi nyingi hutakiwa kubuni jengo imara la watoto kuendelea na kukuwa maishani. Lakini sehemu ya familia inapoanguka, watoto huwachwa na ukosefu wa umadhubuti na kuwasababishia kukukosa mtizamo muhimu wa utotoni ambao ni muhimu kwa maisha.

**Mahusiano na Wazazi:**

Athari kubwa inayopatikana kwa watoto baada ya familia kuvunjika ni wao kukosa mahusiano na mmoja au wazazi wote.

Kwa mfano, wazazi wanapotengana, watoto mara nyingi hukulia ndani ya familia ya “mzazi mmoja” ambapo mara nyingi zimepelekea kupunguza au kupoteza mawasiliano na mmoja wa wazazi. Huko Uingereza na Marekani thumuni moja ya watoto wanalelewa bila baba yao mzazi (Afisi ya Takwimu Marekani na Afisi

*Endelea Uk..10*

ya Takwimu ya Uingereza). Uingereza takribani watoto milioni moja wanakuwa bila kuwepo kwa baba katika maisha yao (CSJ). Takwimu hizi zimekuwa zakushtusha zaidi wakati ambapo utafiti wa hivi majuzi uliofanywa na Harry Benson, Mkurugenzi wa Mawasiliano katika shirika hilo la Uingereza la Msingi wa Ndoa, unaonyesha kuwa "kukosekana kwa baba ndani ya nyumba imebakia kuwa chanzo nambari moja katika kutabiri matatizo ya kiakili kwa vijana ndani ya Uingereza." Iko wazi kuwa watoto wanapokuwa bila baba ndiyo inayowapelekea kuwa dhaifu kwa ujumla.

Ikiwa haitoshi kwa watoto wengi kuwa na mawasiliano na mmoja wa wazazi yatakuwa machache au kukosekana kabisa baada ya kuvunjika, basi pia kuna ushahidi kuwa mahusiano na mzazi ambaye watoto wanakulia naye, hupungua kwa vigezo kadhaa. Kwa mujibu wa (Pryor, J. and Rodgers, B. (2001) Children in Changing Families. Oxford: Blackwell) Moja katika vigezo ni mahitaji ya mzazi mmoja, mara nyingi mama, kwa kuwa mtafutaji mkate wa familia kiasi kwamba hulazimishwa kuwakabidhi watoto wao katika mikono ya wengine kuwaangalia na mara nyingi kuwalea kutokana na majukumu ya kikazi. Huku sehemu ya familia inapokuwa ndogo kila miaka inavyoendelea watoto wanawachwa katika malezi ya watu wasiokuwa muhimu au wanawachwa kujitafutia wenyewe kama "watoto machokoraa" wanaorudi kutoka shule na kuingia nyumba iliyotupu na wanamotakiwa kujisimamia ikijumuisha kujiandalia chakula. Zaidi ya hayo msongo wa mawazo kwa baba na mama uko juu kutokana na talaka, hii ikipelekea mihemko zaidi kwa mahusiano ya mtoto na mzazi.

**Athari Mbaya ya Kiuchumi:**

Baada ya kuvunjika kwa familia, hali ya kiuchumi ya watoto hubadilika kimsingi.

Utafiti uliofanywa Marekani unaonyesha kuwa mama mlezi anapata hasara ya kati ya asilimia 25-60 ya mapata yake kabla talaka. Kina mama asilimia 50 walipata makubaliano ya msaada kwa watoto na asilimia 25 ya kina mama ambao kihakika walikubaliwa kupewa msaada, hawakupata malipo. (US Census Bureau. 2011. Divorce Rates Highest in the South, Lowest in the Northeast, Census Bureau Reports United States Census Bureau Web Site.) Uingereza familia za mzazi mmoja ndizo ambazo zinatarajiwa kuishi katika umasikini wa kifedha. Wazazi pweke wanatarajiwa kuishi mara 2.5 zaidi chini ya asilimia 60 ya mapato ya kati na kati. Asilimia 41 ya watoto kutoka kwa familia za wazazi pweke wanaishi chini ya asilimia 60 ya mapato ya kati na kati baada ya gharama za nyumba. (CSJ, Fractured Families) Kumnukuu mwalimu kutoka Uingereza kinachomaanisha kutoka mashinani: "Tunawaona watoto wasiokula kabla muda wa mchana. Wengi hawawezi kumiliki sare na viatu. Na wengi wanawalea wadogo zao peke yao." Watoto wanaoishi katika umasikini ni takribani mara mbili zaidi wanaotarajiwa kuishi katika nyumba mbaya. Hili lina athari kubwa juu ya miili na akili zao pamoja na kufaulu kwao kielimu.

**Athari za Kijamii, Kihisia, Kiuwezo wa Kitabia na Afya ya Kiakili Juu ya Mtoto:**

Kama jamii tunahitaji kufahamu kwamba katika mahusiano mengi tofauti tofauti ambayo watu huwanayo kwa muda wa maisha yao, mahusiano kati ya mzazi na mtoto ni moja miongoni mwa ambayo ni muhimu. Namna wazazi wanavyotendeana na wanavyowatendea watoto wao, itakuwa ni kiashiria kikubwa cha namna watakavyokuwa ukubwani na dori watayoweza kucheza katika jamii. Huku mahusiano kati ya mzazi na mtoto yanapozidi kudorora kutokana na hali ya familia, tunaona kwamba watoto kutoka katika familia zilizovunjika wanapoteza kwa ujumla hisia ya kustahiki kuwa sehemu fulani. Hisia hii inamaanisha kujihisi kukubalika na kuthaminiwa kama mwanachama au sehemu ya kitu. Ni fikra muhimu tunayohitaji kuihisi ili tuweze kuyaendea masuala yanayotuzunguka na kupambana na mazito maishani mwetu.

Wajuzi wamependekeza kuwa fikra hii muhimu inakosekana ndani ya vijana wengi kutoka katika majumba yaliyovunjika na ndiyo kigezo kikubwa kinachopelekea vijana kuingia katika magenge. Inaweza kuwa sababu ya kwa nini tunaona ongezeko la uhalifu wa magenge. Vijana wengi wanaona kuwa uanachama katika magenge ni kama mbadala wa familia na yanayowapatia hisia hiyo ya kustahiki kuwepo sehemu fulani. Katika mahojiano na wanachama wa magenge kutoka Marekani, yaliyofanywa na Joe Killian, muandishi wa News and Record, wanachama wengi walisema kwamba, "Kuwa ni sehemu ya genge inamaanisha kuwa hauko peke yako katika dunia, ambayo ni sawa na vile watu wengi wanavyoelezea kuwa ni sehemu ya familia iliyoshikamana au kundi la marafiki."
Zaidi ya hayo, uamuzi ufuatao ulipeperushwa katika ripoti na Muungano wa Kitaifa wa Uingereza wa Muungano wa Wakuu wa Shule wa Walimu wa Kike uliosisitiza dori ya kuvunjika kwa familia kuwa ndiyo imepelekea kukua kwa tamaduni za magenge ndani ya Uingereza. Ilisema kwamba kuvunjika kwa familia na kukosekana kwa baba kama msimamizi inawezekana kulaumiwa kuwa chanzo cha wanafunzi kujiunga na magenge, "Watoto wa umri wa miaka tisa wanahusishwa na uhalifu wa kupangiliwa ili wapate kuhifadhiwa na kupata "hisia ya kustahiki kuwa sehemu" kwa sababu ya kukosekana viigizo kutoka nyumbani."

Hali ya ustawi jumla ya watoto pia inaathiriwa kutokana na familia zao kuvunjika. Ilipatikana kuwa ustawi jumla wa watoto kutoka katika nyumba zilizovunjika uko chini ikilinganishwa na watoto wanaotoka katika familia za wazazi wawili. Tathmini kubwa juu ya watoto wa wazazi walio talakiana ya (Amato 1991 and 2001: Children of divorce in the 1990s: an update of the Amato and Keith

*Endelea Uk..11*

(1991) meta-analysis. Journal of Family Psychology,15, 355-70) iligundua kuwa watoto kutoka katika familia za talaka walikuwa na kiwango cha chini kutokana na athari ikijumuisha kufaulu kielimu, kitabia, marekebisho ya kisaikolojia (kiakili), dhana ya kibinafsi, uwezo wa kijamii na afya ya muda mrefu. Katika utafiti mwengine, ushahidi uligundua kuwa watoto kutoka kwa wazazi waliotengana wanauwezekano mkubwa wa kupata matatizo ya kitabia na wanaweza kufanya vibaya shule na kuacha shule wakiwa na viwango vya chini vya kuhitimu. (Pryor, J. and Rodgers, B. (2001) Children in Changing Families. Oxford: Blackwell). Utafiti mwengine ni kuwa watoto ambao wazazi walio talakiana wanaweza kuwa na viwango vya chini juu ya dhana ya binafsi na mahusiano ya kijamii (Amato 2001) na kwamba wasiwasi na msongo wa mawazo huzidi baada ya tukio la talaka (Strohschein 2005Parental divorce and child mental health trajectories. Journal of Marriage and Family 67: 1286.)

Mzigo wa familia kuvunjika juu ya ujumla wa maendeleo ya hisia kwa watoto pia iliwekwa wazi na utafiti uliofanywa Sweden ambapo takribani watoto milioni moja ulionyesha kuwa watoto wanaokuwa wakiwa na wazazi pweke wanauwezo wa kupata mapungufu ya kiakili makubwa, kujaribu au kujitoa uhai au kudumu na kunywa pombe. Takwimu za kushtusha kutoka Marekani juu ya athari ya kukosekana baba nyumbani na maendeleo ya watoto zimeonyesha namna gani tatizo lilivyokubwa. Kwa mfano Marekani asilimia 63 ya vijana wanaojitoa uhai wanatoka katika nyumba zisizokuwa na baba (US Department of Health) na watoto wa kutoka nyumba za wazazi pweke ni mara mbili zaidi kuwa wanauwezo wa kujitoa uhai (Irwin Sandler, PhD, professor of psychology and director of the Prevention Research Center, Arizona State University, Tempe). Zaidi ya hayo, utafiti wa watoto 1,977 wa umri wa miaka 3 na zaidi wanaoishi na baba nyumbani au msimamizi kama baba iligundua kuwa watoto wanaoishi na wazazi wadamu waliooana walikuwa na kiwango cha chini cha matatizo ya kitabia katika kujieleza na kujiamulia kuliko watoto wanaoishi na mzazi mmoja asiyekuwa wa damu. (Hofferth, S. L. (2006). Residential father family type and child well-being: investment versus selection. Demography, 43, 53-78.). Pia kuna matumizi makubwa ya madawa ya kulevya kwa watoto wasioishi na baba na mama yao. (Hoffmann, John P. “The Community Context of Family Structure and Adolescent Drug Use.” Journal of Marriage and Family 64 (May 2002): 314-330.)

Zaidi ya hayo, utathmini wa takribani familia 11,000 uliyofanyika ndani ya Uingereza uligundua kuwa kuvunjika kwa familia ndiyo chanzo hatari cha kipekee kwa afya ya kiakili kwa watoto wanapo baleghe na kuwepo kwa wazazi waliotengana ni athari kubwa ya kipekee juu ya afya ya kiakili kwa wasichana hususan matatizo ya kihisia. Na kwa pamoja ni kigezo kikubwa katika afya ya kiakili ya vijana ikiwa na mahusiano ya matatizo ya kitabia (The Times)

Imesemekana kuwa kuzidi kwa maradhi ya kiakili ni kutokana na kukosekana kwa furaha ndani ya jamii. Huku idadi ya msongo wa mawazo na wasiwasi miongoni mwa vijana, na idadi ya watoto na vijana wanaozuru ndani ya kitengo cha Ajali na Dharura (A&E) wakiwa na matatizo ya kiakili ikizidi ndani ya miaka 10 na huku idadi ya wanaosajiliwa hospitalini katika vijana walio na matatizo ya kula ikizidi. (The Independent) Serikali kamwe haziwezi kupinga kuzidi kwa idadi ya vijana ambao wameathirika kihisia na kiakili kutokana na kuvunjika kwa familia na kinachoashiriwa ni kuhusu maadili na mwenendo wa maisha ya jamii ambazo serikali hizi zinatawala juu yake.

Katika jamii zote za kimagharibi, familia pana zimepotea kabisa, na kwamba utamaduni wa wazazi wawili umezidi kupungua kutokana na idadi kubwa ya talaka, kuoana tena, kuchukuana, uzazi wa upweke na mahusiano ya jinsia moja yote yamezidi. Matokeo ya mabadiliko haya juu ya jamii kiujumla hususan maisha ya watoto yamekuwa yakushtusha. Ilhali serikali zajitia hamnazo katika kutoa suluhisho. Hili si la kushangaza kwa kuwa ndiyo maadili huru ya kisekula na nidhamu wanazopigia debe na kutekeleza juu ya dola zao na ambazo zimesababisha michafuko katika jamii. Lakusikitisha, inatarajiwa kuwa maangamivu yanayotokana na kuvunjika kwa familia yataendelea na hata kuzidi katika miaka ijayo, ikimakinisha mahangaiko kwa wengi hususan wachanga.

**Yasmin Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 18: Utafutaji wa Nusra ni Amri Kutoka kwa Allah (swt) Inapasa Kusimama Nayo; ni Sehemu Katika Njia (Twariqa) ya Kisheria, Haifai Kuikataa Wala Kuidharau

Katika Halaqa hii tutaangalia utafutaji wa nusra ni amri kutoka kwa Allah (swt) inapasa kusimama nayo; ni sehemu katika njia (twariqa) ya kisheria, haifai kuikataa wala kuidharau.

Tunatilia mkazo kuwa utafutaji wa nusra sio rai ama mbinu ambazo ameonelea Mtume (saw) kuzifanya kwa mapenzi ya nafsi yake, bali ni amri kutoka kwa Allah (swt) na ni lazima kwa Rasul (saw) kuitekeleza. Na dalili juu ya hayo ni katika Kitabu na Sunnah, na elimu ya usul.

Kwanza: katika Kitabu:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۚ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِي

Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjue anaye mnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda. [Surat Al-Hadid: 25]

Hakika ametupa khabari Mola wetu (swt) ya kwamba ametuma Malaika kwa Manabii na kwa Mitume, na akawatuma hawa Manabii na Mitume kwa ummah, na akawapa nguvu kwa miujiza ya wazi, na hoja za wazi, na akawateremshia vitabu ili abainishe haki, na awapambanulie watu usawa ili wawafuate.

Allah Tabaraka wa Ta'ala akaweka katika ardhi mizani ya haki na uadilifu; ili ziwekwe sawa haki, na usimamishwe kwayo Uadilifu. Na Allah akateremsha chuma chenye nguvu nyingi, ili zipatikane ala za kivita ambazo watatumia Waislamu kuinusuru Dini ya Allah na Mitume ya Allah, na hilo ni kwa kuzitumia hizi silaha za nguvu katika kuwapiga Vita/Jihad makafiri, na kuwazuia wenye nafsi za maradhi, ambao wamekengeuka Manhaj ya Allah, na wakavuka mipaka katika haki za waja wa Allah.

Hakika Allah Subhanahu wa Ta'ala ametubainishia hikma ya hayo yote, amebainisha hikma ya kutuma Mitume, na kuteremsha vitabu na mizani na kuteremsha chuma, nayo ni mtihani kwa mwanadamu. Je, atasimama upande wa haki, kisimamo cha mwenye kuinusuru Da'wah na Manhaj ya Allah..? Ama atasimama pamoja na watu wa batili kisimamo cha mwenye kumpinga Allah na Mtume wake, adui anayeipiga vita Da'wah na Manhaj ya Allah? Na ilhali Allah ndiye wa haki naye ni Mwenye nguvu Mwenye kuweza kumwangamamiza amtakaye, na Allah (swt) ni Mwenye nguvu ambaye hahitaji msaada wa yeyote katika wanadamu, bali Yeye kawaamrisha Jihad; ili wanufaike nayo, na wapate Thawabu kwa kufuata Amri za Allah.

Kwa yote yaliyo tangulia, na kwa maf'hum ya aya tukufu na kwa mantiki yake, inabainika kwamba Haki haina budi ipate nguvu itakayo inusuru na kuihami, kwa sababu hiyo tunamuona Mtume (saw) kama tunavyo elezwa na vitabu vya seera, anatoka na kwenda Twaif akitafuta Nusra kwa Thaqif pamoja na hifadhi, akitaraji watamkubalia kwa alichokuja nacho kutoka kwa Allah Azza wa Jalla, isipokuwa wao hawakumkubalia, wakawatuma wajinga wao na watumwa wao wamcheshere Mtume (saw).

Akaendelea Rasul (saw) akijitambulisha kwa makabila, na kuwatafuta wenye nguvu (Ahlil Quwwa), mpaka Allah akamneemesha kwa Nusra na uungwaji mkono.

Pili: Katika Sunnah ni kitendo cha Mtume (saw):

Amepokea Abu Nuaim kutoka kwa Ali bin Abi Twalib (ra) asema: (Allah Alipomuamrisha Mtume wake ajitambulishe kwa makabila ya Waarabu, alitoka na mimi na Abu Bakar mpaka tukafika Minaa, tukatokea katika kikao cha Waarabu, akatangulia Abu Bakar (ra) akasalimia, na alikuwa Abu Bakar anatangulia kwa kila kheri, na alikuwa mtu mwenye Nasaba.

Tatu: Ni katika elimu ya usul:

Inatoa ufahamu kuwa kutaka kitu kifanywe (طلب الفعل) kisha kile kitu kikakaririwa kutaka kifanywe (وطلب تكراره) pamoja na kuwa jambo ni zito (مع المشقة) basi ni kiashiria (Qarina) miongoni mwa Qarina za kuwajibisha. (هو قرينة من قرائن الجزم في خطاب التكليف)

Anasema mwanachuoni Ata Abu Rashtah katika kitabu chake "Taysirul wusul ilal usul":
(ومن صيغة الطلب والقرينة الجازمة يكون حكم هذا الفعل الوجوب). (Na kutokana na matamshi ya kutaka kitu kifanywe na qarina ya kulazimisha (Al-Jaazimah), hukmu ya kitendo inakuwa wajib)

Na inajulikana kuwa Rasul (saw) alijitambulisha kwa makabila karibu mara ishirini na moja (21) Na kwa hayo hakika hiki kitendo cha Mtume (saw) kukirudia mara nyingi pamoja na uzito ulio katika hiki kitendo, ambapo watu wa Twaif walimuudhi, wakampiga mawe mpaka nyanyo zake tukufu zikajaa damu, hii inamaanisha kutafuta Nusra ni wajib. Kwani lau si wajib Mtume (saw) asinge kakamia kiasi hiki kitendo hichi.


Email: info@uqab.or.ke

# SWALI/JAWABU:
# Msisitizo wa Trump Juu ya OPEC, Hususan Juu ya Saudi Arabia, ili Kuongeza Uzalishaji na Kupunguza Bei za Mafuta

**Swali:** Mnamo 2 Oktoba 2018, wakati wa mkutano wa uchaguzi wa muhula wa kati katika eneo bunge la Mississippi, Trump aliitishia Saudi Arabia na kuwaonyesha wafuasi wake kuwa alikuwa akipambana na bei za juu za mafuta: **"… Na vipi kuhusu mikataba yetu ya kijeshi ambapo tunalinda mataifa tajiri na hatulipwi, vipi kuhusu hiyo mali "kwa maana ya mafuta"? Ambayo pia inabadilika… Tunailinda Saudi Arabia. Je, mutasema kuwa wao ni matajiri? Na nampenda Mfalme, Mfalme Salman. Lakini nilisema 'Mfalme – sisi tunakulinda – huenda usiwepo hapo mamlakani kwa wiki mbili bila ya sisi – ni sharti ulipe kwa ajili ya ulinzi wako.'"** (Khaleej Online, 03/10/2018).

Swali langu sio ni kwa nini watawala wa Saudi Arabia wanasalia kimya juu ya tusi hili, bali wamesalia watiifu kwa Amerika, ni kwa sababu ni wadogo machoni mwao wenyewe, na hivyo wamekulia wakizoea fedheha. Lakini swali langu ni kipi kinachomfanya Trump kuifuatilia Saudi Arabia kwa pupa ili kuongeza uzalishaji na kupunguza bei; ingawa Amerika ni mzalishaji mkubwa na inaweza kudhibiti upunguzaji bei yeye peke yake? Sasa kwa nini inasisitiza wakati huu? Na hatimaye, kwa nini, licha ya shinikizo hili lote la Amerika bei ya mafuta haijapungua? Na Allah akulipe kheri.

**Jibu:** Ndiyo, umesema ukweli, anaye fedheheshwa amezoea kufedheheshwa, taarifa za Trump kuhusu watawala wa Saudi Arabia zatosha kuyaangamiza mahusiano na Amerika, ikiwa si juu ya hilo, bali ikiwa wanamuonea haya Allah, Mtume wake na waumini, lakini hawana haya, na Mtume wa kweli (saw) amesema:**«إِنَّ مِمَّا أَدْرَكَ النَّاسُ مِنْ كَلَامِ النُّبُوَّةِ إِذَا لَمْ تَسْتَحْيِ فَاصْنَعْ مَا شِئْتَ»**"Hakika, miongoni mwa yale ambayo watu wameyatambua kutoka katika maneno ya mitume ni: ikiwa huna haya, basi fanya utakavyo."[Al-Bukhari]

**Ama kuhusu jibu la swali lako au maswali yako, ni kama ifuatavyo:**

1. Pindi Trump alipoingia afisini mnamo Januari 2017, bei za mafuta zilikuwa takriban $57 kwa pipa. Kufikia Juni 2017, bei za mafuta zilishuka hadi $45 kwa pipa, lakini tangu hapo zimeendelea kupanda. Leo, bei ya mafuta ni $86 kwa pipa la mafuta ghafi na baadhi ya wadadisi wanatarajia bei za mafuta kufikia $100 kwa pipa!

Mnamo 5/7/2018, Trump aliandika katika mtandao wa Twitter: **"Shirika la kikiritimba la OPEC ni lazima likumbuke kuwa bei za gesi ziko juu na wanafanya juhudi chache kusaidia. Kama kuna chochote, basi wanazisukuma bei juu zaidi huku Amerika ikiwatetea wengi wa wanachama wake (yaani wanachama wa OPEC) kwa dolari chache. (Uhusiano) huu ni lazima uwe wa pande mbili (yaani tunawasaidia kwa badali ya bei ya chini ya mafuta) … PUNGUZENI BEI SASA!"** Kabla ya hapo mnamo 30 Juni 2018 alisema katika maandishi yake katika mtandao wa Twitter: **"Hivi punde nimezungumza na Mfalme Salman wa Saudi Arabia na kumweleza kuwa, kwa sababu ya ghasia na sokomoko nchini Iran na Venezuela, naiomba Saudi Arabia iongeze uzalishaji mafuta, pengine hadi mapipa 2,000,000, ili kufidia tofauti … Bei ziko juu sana! Amekubali!"** (Al-Hura: 30/6/2018)

Mnamo 25/9/2018 Raisi wa Amerika aliishambulia OPEC katika hotuba yake katika Kongamano Kuu la UN na kusema: **"OPEC na mataifa ya OPEC, kama kawaida, yanauvuna ulimwengu wote, na hili silipendi. Hakuna yeyote anayepaswa kulipenda hili. Tunayapa ulinzi mengi ya mataifa haya bure bilashi, na kisha kututumia kwa kutupa bei za juu za mafuta … tunawataka waanze kupunguza bei … Hatutazivumilia tena bei hizi mbaya."** (Sputnik, Septemba 25, 2018), na mnamo 27/9/2018, Trump aliandika katika mtandao wa Twitter **"Tunazipa ulinzi nchi za Mashariki ya Kati, haziwezi kuwa salama kwa muda mrefu bila ya sisi, na huku zinaendelea kusukuma bei za mafuta juu na juu zaidi! Tutakumbuka. Shirika la kikiritimba la OPEC ni lazima lishukishe bei sasa!"**

Kama ilivyoelezwa katika jibu la swali mnamo 2/10/2018 katika muhula wa kati wa mkutano wa kampeni ya uchaguzi katika eneo bunge la Mississippi, Trump ameitishia Saudi Arabia na kuwaonyesha wafuasi wake kuwa anakabiliana na ongezeko la bei: **"… Na vipi kuhusu mikataba yetu ya kijeshi ambapo tunayalinda mataifa tajiri na hatupati malipo, vipi kuhusu bidhaa hiyo "yaani mafuta"? Hilo pia linabadilika wenzangu … Tunailinda Saudi Arabia. Je, utasema wao ni matajiri. Na nampenda Mfalme, Mfalme Salman. Lakini nilimwambia 'Mfalme – sisi tunakulinda – huenda usiweko mamlakani kwa wiki mbili tu bila ya sisi – ni lazima ulipie ulinzi wako." (Khaleej Online, 03/10/2018).**

**Yote haya yamaanisha kuwa kinachomtia wasiwasi Trump, ni hali zilizoko sasa, katika kuongeza uzalishaji, lakini kutoka OPEC, hususan kutoka Saudi Arabia.**

2. Ndiyo, Amerika ndiyo mzalishaji mkubwa zaidi, kwa mujibu wa Idara ya Habari za Kawi ya Amerika (EIA), shirika la Amerika linayokusanya takwimu za kawi. Mwishoni mwa 2017, EIA ilichapisha jedwali la uzalishaji wa mafuta duniani, ambapo wakati huo ilikuwa ni mapipa

*Endelea Uk..14*

milioni 95 kwa siku. Kwa mujibu wa jedwali hilo, nchi saba zinazoongoza kwa uzalishaji ni kama zifuatazo:

Amerika: mapipa milioni 14.46 kwa siku ya jumla ya uzalishaji wote duniani, Saudi Arabia: milioni 12.08, Urusi: milioni 11.18, Canada: milioni 4.87, Iran: milioni 4.67, Iraq: milioni 4.48, China: milioni 4.45.

**Amerika inabakia kuwa mzalishaji mkuu wa mafuta duniani, ikifuatiwa na Saudi Arabia na Urusi**

3 – Na ndiyo, Amerika inaweza kuongeza uzalishaji kama ipendavyo, hususan kwa kuwa ina akiba kubwa ya mafuta ya shale, lakini kuna kitu kinachoizuia kufanya hivyo:

a – Kudumisha akiba na hifadhi zake

b – Kuna Ruwaibidha (watawala waovu) wanaotekeleza maagizo yake hata kama wanatusiwa katika jambo hili. Wao hata hutekeleza hili huku likiwa na madhara kwao, kama ilivyo kwa watawala wa Saudi Arabia!! Amerika inaitaka Saudi Arabia kupunguza bei za mafuta ili kuwapa watu wake bei za chini kabisa baada ya bei ya mafuta ghafi ya Brent kufikia kiwango cha kiulimwengu cha takriban $80 kwa pipa katika mwezi wa tisa mwaka huu. **"Mnamo 14/9/2018 kiwango cha kiulimwengu cha mafuta ghafi ya Brent kiliongezeka na kuwa $78.21 kwa pipa, ongezeko la juu zaidi tangu 22/5/2018" … (Reuters 14/9/2018). Tambua kuwa "uzalishaji wa OPEC uliongezeka hadi mapipa milioni 32.79 kwa siku. Saudi Arabia, iliyo ahidi dhamira ya ongezeko katika uzalishaji wake, ilisema kuwa uamuzi huo utapelekea ongezeko la uzalishaji kwa takriban mapipa milioni moja kwa siku" (Reuters, 31/8/2018). "Pindi mafuta ghafi ya Brent yalipokuwa yakielekea $80 kwa pipa, Saudi Arabia iliiliarifu soko kuhusu kuongeza uzalishaji wake mwezi uliopita mapema kuliko tarehe ambayo habari hiyo kwa kawaida hutangazwa,"** imenukuliwa kutoka chanzo chake.

Serikali ya Saudi ni kibaraka imara wa Amerika na iko kuihudumia. Saudi Arabia daima imecheza dori muhimu sana katika kuimarisha soko la mafuta … Saudi Arabia, inahitaji bei za juu za mafuta wakati huu, ambapo uchumi wake uko katika shinikizo hatari la kiuchumi tangu kuanguka kwa bei ya mafuta mnamo 2014. Hususan kwa kuwa mafuta ndiyo pato kuu katika bajeti ya Saudi Arabia. Ni maarufu kuwa katika nchi ambazo mapato ya mafuta yanajumuisha zaidi ya nusu ya mapato yao, wanahitaji bei za mafuta ziwe juu ya $80 kwa pipa kuweka uzani sawa wa bajeti yao – mapato ya kutosha ya mafuta ili kumudu matumizi ya bajeti – hali iko vipi ikiwa bajeti ya Saudi Arabia imejengwa kikamilifu juu ya mapato ya mafuta? Bei maridhawa iko juu ya $80, hata karibu na $100 ili kuweka mizani sawa bajeti yake, na kuimarisha uchumi wake, kwani kwa sasa unayumba. Lakini, mtawala wake anakubali kuongeza uzalishaji ili kupunguza bei, bila ya kujali madhara yanayofanyiwa nchi hiyo ili kumridhisha Trump, ambaye amemtusi mtawala wa Saudi hadharani, kuwa lau si Amerika, utawala wake ungekuwa umeporomoka!! Wanalifungia macho hili na mfalme wao mtarajiwa kusema kuwa Saudi Arabia iko tayari kufidia upungufu wa Iran! Mnamo 6/10/2018 Shirika la Habari la Bloomberg liliripoti taarifa za mfalme huyo mtarajiwa Bin Salman: **Alisisitiza kuwa Saudi Arabia imetimiza ahadi yake ili kufidia kutoweka kwa usambazaji mafuta ghafi wa Iran," na akasema: "Saudi Arabia kwa sasa inazalisha takriban mapipa milioni 10.7 kwa siku – karibu na rekodi – na kuongeza milioni 1.3 zaidi endapo soko litahitajia hilo …"**

Maadamu kuna kibaraka wa Amerika aliye tayari kujidhuru ili kufikia matakwa ya Trump ya kuongeza uzalishaji, ni kwa nini basi Amerika itumie hifadhi zake?

4- Kwa nini msisitizo huu wa Trump kwa OPEC, na hususan Saudi Arabia ili kuongeza uzalishaji na kupunguza bei? Ni kwa sababu kuna vitu viwili vinavyo jumuisha kizungumkuti cha haraka kwa Trump ambaye anataka kitatuliwe kwa haraka, vyenginevyo Trump haathiriwi na ongezeko la bei … Amerika yaweza kudhibiti ongezeko hilo kupitia kuchapisha dolari mpya, kama ilivyo fanya pindi kulipokuwa na ongezeko la nyuma la bei kwa takriban $150. Tulitoa katika jibu la nyuma la swali mnamo 16/5/2009: **"kwamba Amerika yaweza kuchapisha noti, kwa idhini ya Hazina ya Fedha Ulimwenguni (IMF) au kwa siri, "hata hadharani" bila ya ridhaa yake, kwa kuwa ina ushawishi imara katika Hazina hiyo, na yaweza kuonyesha sababu za kirongo na kuficha ukweli wa mambo, na yaweza kupata usaidizi wa Hazina hiyo! Lakini uchapishaji wa noti kwa njia hii hupelekea kushuka thamani kwa dolari, na mkurupuko wa bei, yaani ongezeko la bei. Hii ndiyo sababu Amerika haichukui hatua hii isipokuwa ikiwa ina maslahi ndani yake. Kwa mfano, imeripotiwa kuwa Amerika ilichapisha kati ya "trilioni 2 – trilioni 4" wakati wa shauku ya mafuta, iliyo sababisha ongezeko la bei kwa karibu $150 kwa pipa, "na Amerika haikuwa mbali na shauku hiyo". Amerika ilichapisha noti hizi ili kununua kiwango kikubwa kabisa cha mafuta kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja ili kuongeza akiba yake, ililiona hili kuwa la manufaa kuliko bei za juu na kuporomoka kwa dolari …"** lakini kwa sababu inachukua muda kupangilia uzalishaji wa "mandhari" hii! Na kwa sababu kadhia mbili hizi zahitaji suluhisho la haraka au vyenginevyo Trump ataanguka ndani ya matatizo kama tulivyo taja awali. Hivyo, Trump alighadhabishwa na OPEC, na hususan Saudi Arabia … Hivi ndivyo vizungumkuti viwili:

**Cha kwanza: Kadhia ya vikwazo juu ya Iran:**

Iran ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mafuta ghafi katika OPEC baada ya Saudi Arabia na Iraq, uzalishaji wake

*Endelea Uk..15*

ni takriban mapipa milioni 4 ya mafuta ghafi kwa siku. Vikwazo hivyo vitapelekea uhaba wa usafirishaji mafuta ya Iran, hususan mnamo Novemba, ambapo vikwazo vinaongezeka ikiwemo Iran pamoja na waagizaji mafuta kutoka Iran. Amerika imeziagiza kampuni kukata uagizaji mafuta kutoka Iran kwanza, na kisha kufutilia mbali mikataba yao na Iran Novemba ijayo, itakayo pelekea kupungua kwa ushafirishaji bidhaa ng'ambo wa Iran. Lakini Saudi Arabia yaweza kuongeza uzalishaji wake wa mafuta endapo kuna haja, maana yake ni kuwa imejitayarisha kufidia uhaba wa usambazaji wa Iran. Mfalme Mtarajiwa wa Saudi Mohammad bin Salman alisema: **"Hivi karibuni tunasafirisha kadri ya mapipa mawili kwa pipa lolote linalopotea kutoka Iran," mwanamfalme huyo alisema. "Kwa hivyo tumefanya kazi yetu na zaidi." Kwa sasa Saudi Arabia inatoa takriban mapipa milioni 10.7 kwa siku – karibu na rekodi – na yaweza kuongeza milioni 1.3 zaidi endapo soko litahitaji hilo."** (https://www.akhbarak.net, 08/10/2018).

Mnamo 4/11/2018, Amerika inapanga kuongeza vikwazo dhidi ya Iran, ikilenga usafirishaji mafuta ng'ambo na kuzitia shinikizo serikali na makampuni kote ulimwenguni kuzingatia na kupunguza ununuzi kutoka Iran. Hii yamaanisha kuwa usambazaji mafuta utapungua katika soko la kiulimwengu. Kama ilivyo taarifa ya nchi saba kuu za uzalishaji mafuta iliyotajwa juu, Iran ilikuwa ikizalisha zaidi ya mapipa milioni 4 ya mafuta kwa siku" na sasa hii imeshuka." Nusu ya mafuta hayo ndiyo yanayo zalishwa, China, India na Uturuki, hupokea kutoka kwake karibia mapipa milioni 2. Trump anataraji hatua za vikwazo hivyo zitaondoa milioni 2 hiyo. Amerika inataka kuifidia kupitia Saudi Arabia na nchi nyengine za OPEC kufidia upungufu huo unaotarajiwa, ili Amerika iweze kuwasilisha kadhia ya Iran kando na Ulaya, Urusi na China baada ya kutangaza kujiondoa kwake mnamo 8/5/2018 kutoka katika makubaliano ya nuklia yaliyotiwa saini miaka mitatu iliyopita na nchi hizi. Ilikubali makubaliano na Iran pekee. Raisi wa Amerika ametangaza kuwa tayari kwake kufanya makubaliano kama hayo, lakini masharti yake ni lazima yaundwe ndani ya Iran. Hili laweza kuchukua muda mrefu … Trump anataka kufidia uhaba huu hadi pale atakapo weza kuandaa makubaliano kati ya Amerika na Iran bila ya kuihusisha Ulaya, endapo uhaba huo utaendelea kuwepo bila ya fidia na kisha bei kuongezeka, hili litamueka yeye matatani. Kwa sababu yeye ndiye aliyeunda vikwazo hivyo kwamba ukosefu wa mafuta ya Iran kama natija ya vikwazo hivyo itafidiwa na vitisho vyake kwa OPEC, hususan Saudi Arabia … kwa maana nyengine, Amerika inataka kuwasilisha kadhia ya ukosefu wa usambazaji wa mafuta na kuhakikisha kuwa hautokei hadi matatizo haya na Iran yatatuliwe, kwa sababu hili huenda lisiwe kwa haraka.

Hivyo basi, Trump anaisisitiza OPEC na kimsingi Saudi Arabia kufidia upungufu wa usambazaji wa Iran, ambao utakuwa dhahiri mnamo 4/11/2018, ikiongezewa na upungufu uliosababishwa na vikwazo mnamo 21/05/2018 vilivyo wekwa na Trump juu ya Venezuela, hata kama ushawishi wake ni mchache. uzalishaji wake wa sasa ni mapipa milioni 1.5 kwa siku.

**Cha pili ni uchaguzi wa Amerika:**

Kupandisha bei za mafuta humsababishia Donald Trump, ambaye atasimamia uchaguzi wa muhula wa kati mnamo Novemba. Bei za juu za mafuta zitawaweka wafuasi wake afisini, hususan kwa kuwa kura nyingi za maoni zaonyesha kuwa Democrats watalidhibiti Bunge. Ili kuwaonyesha wapiga kura wa Amerika kuwa anaiweka Amerika mbele, anaweka lawama na shinikizo juu ya Saudi Arabia na wanachama wa OPEC ili kuongeza uzalishaji. Wakati huo huo, utawala wa Trump unailazimisha China, India na Uturuki kuvunja mafungamano na Iran na kutafuta mafuta ghafi kwengineko. Ongezeko la bei za mafuta pia la athiri kiasi cha bei ambayo wanunuzi wa Amerika wanalipia mafuta. Kwa uchaguzi huu wa muhula wa kati, hili halitakuwa jambo la kushindia. Hisia za Waamerika kwa ongezeko la bei za mafuta ziko juu, na hawawezi kukubali kuwa serikali yao iongeze bei za mafuta, kwa hivyo Raisi Trump anarusha lawama ya bei za juu kwa dola za Ghuba na OPEC na kuzishambulia ili kuwaonyesha Waamerika kuwa anatetea maslahi yake na anaweza kuishinikiza Saudi Arabia na OPEC ili kupunguza bei. Ameshughulishwa na kushukisha bei hiyo, hususan katika kipindi cha uchaguzi wa Amerika. Hili ni muhimu leo kwa Raisi wa Amerika na mahitaji ya chama chake cha Republican ili kupata kura za wapiga kura wa Amerika katika uchaguzi wa muhula wa kati wa Novemba 6, 2018 hususan kwa kuwa kura za maoni zinawafadhilisha Democrats.

5- Ni kwa nini bei za mafuta zaendelea kuongezeka licha ya vitisho vya Trump na shinikizo lake na jibu la Saudi Arabia? Sababu ni kuwa kuna wahusika wengine katika OPEC wafuasi wa Ulaya na katika mzozo na Amerika, na kuna Urusi vile vile, na pande hizi, hususan zile zinazo nasibishwa na Ulaya, si rahisi kuijibu Amerika isipokuwa kwa kiwango ambacho hakitafikia matarajio ya Trump kwa haraka kama anavyotaka. Saudi Arabia ni ala kuu ya Amerika ndani ya OPEC, lakini kuna wengine ndani ya OPEC wana maslahi maalumu, wakiwemo wale wafuasi wa nchi kubwa za Ulaya, na huenda wasiitii Amerika kwa urahisi, pamoja na kuwa kuna nchi washirika wa OPEC kama Urusi zilizo na maslahi maalumu. Amerika haiwezi kulazimisha matakwa yake kikamilifu.

Katika jaribio la kupunguza bei, raisi aliagiza kuongezwa kwa uzalishaji. Lakini, OPEC na washirika wake katika uzalishaji hawakufikia makubaliano katika mkutano wao nchini Algeria mnamo 23/9/2018 juu ya kuongeza zaidi katika uzalishaji wa mafuta, kinyume na wito wa Trump.

Ama kuhusu Urusi, Amerika ilifaulu mnamo 2017, na hadi leo kuitumia Saudi Arabia ili kuishinikiza Urusi na kuifedhehesha na kuijibu kwa kuongeza uzalishaji na

*Endelea Uk..16*

kisha kupunguza bei … Ni mara ya kwanza kwa mfalme wa Saudi kuzuru Urusi ili kuhudhuria mkutano mnamo Oktoba, 2017 kati ya OPEC na wanachama wasio wa OPEC, hususan Urusi, mnamo Oktoba 2017, mfalme Salman alizuru Urusi na kuhudhuria mkutano wa OPEC. Bei za mafuta kisha zilianza kumakinika juu ya $60 kwa pipa kabla ya kuongezeka tangu katikati ya mwaka wa 2018, kama ilivyo elezwa awali. Lakini, Saudi Arabia na Urusi ziling'ang'ana kufikia matakwa ya mapipa milioni 2 kwa siku yaliyo agizwa na Trump. Bali, wadadisi huru pamoja na Shirika la Kimataifa la Kawi (IEA) wanashuku kuwa Saudi Arabia na Urusi huenda wakaongeza mapipa milioni 2 kwa siku. Shirika la Kimataifa la Kawi (IEA), kampuni iliyo na makao yake Paris inayo wakilisha nchi wanunuzi, hivi majuzi ilikadiria kile ilichokiita "usambazaji kwa mahitaji madogo" kutoka Mashariki ya Kati, ikiwemo Saudi Arabia, kwa mapipa milioni 1.14 kwa siku.

Urusi huenda ikaongeza hadi mapipa 400,000 kwa siku, wadadisi wanasema. Mwishowe, chini ya shinikizo la kudumu kutoka Amerika, Saudi Arabia ilifikia makubaliano na Urusi mnamo Septemba kuongeza uzalishaji wa mafuta. "Makubaliano hayo yanaeleza kuwa Urusi na Saudi Arabia zinaendelea kutoa uamuzi wa sera za uzalishaji mafuta kabla ya kuwashauri wanachama wengine wa OPEC," duru hizo zilisema kuwa Waziri wa Kawi wa Saudi Khalid al-Falih na mwenzake wa Urusi Alexander Novak walikubaliana wakati wa misururu ya mikutano juu ya kuinua uzalishaji kuanzia Septemba hadi Disemba, huku bei ya mafuta ghafi ikiwa takriban $80 kwa pipa. Duru hiyo ilisema: "Warusi na Wasaudi wamekubaliana kuongeza uzalishaji mafuta sokoni kimya kimya, ili wasionekane kana kwamba wanatekeleza maagizo ya Trump kwa kuzalisha mafuta zaidi." Duru nyengine ilisema: "Waziri wa Saudi alimwambia Waziri wa Kawi wa Amerika Rick Perry kuwa Saudi Arabia itaongeza uzalishaji endapo wateja wake watahitaji mafuta zaidi." (www.reuters.com).

Pengine mtu anashangaa ni kwa nini Urusi ijiunge na Amerika katika kuzuia bei za juu za mafuta, hata ingawa bei za juu ni kwa manufaa ya Urusi? Ili kujibu swali hili, uchunguzi wa ukweli huu waonyesha kuwa Urusi inaunga mkono bei ya mafuta ya $65 kwa pipa, kwa sababu hii ndiyo bei ya mizani sawa ya sekta ya mafuta ya Urusi, bei za juu zitazifanya nchi zinazo agiza mafuta kushindwa kumudu kuyanunua hatimaye kupelekea kuporomoka kwa upande wa kuyahitaji, ambayo itaidhuru sekta ya mafuta ya Urusi.

Kwa hali yoyote ile, Urusi haiko katika hatari kubwa katika hesabu hii, lakini kile kinacho athiri kihakika hesabu hii ni wale wanachama wa OPEC wa mrengo wa Ulaya. Si rahisi kutekeleza yale ambayo Trump anaagiza isipokuwa kwa shinikizo kubwa sana … Lakini, bei hazitarajiwi kuongezeka hadi 100, kwa kuwa nchi zinazo agiza mafuta haziwezi kuhimili hilo, na mahitaji yatashuka na kisha ongezeko hilo kusimama na kuanguka … hamu ya Trump ni kupunguzwa kwa bei wakati wa kipindi cha uchaguzi na baada yake, yaani kufikia mwishoni mwa mwaka huu ambapo haitarajiwi kuwa kadhia ya makubaliano ya nuklia itakuwa imeanza kuelekea katika makubaliano ya pande mbili kati ya Iran na Amerika bila ya Ulaya, na shinikizo la Amerika juu ya ongezeko la uzalishaji litamalizika na hivyo bei kuzunguka katika $80 kwa pipa …

Kinachotia uchungu zaidi ni kuwa nguvu kutoka nje hutumia rasilimali za ulimwengu wa Kiislamu kucheza michezo dhidi ya wao kwa wao, huku watawala wetu Ruwaibidha wakifuata kiupofu sera hizi na pasi na heshima yoyote kwa hadhi ya Umma huu. Tambua kuwa hifadhi nyingi za mafuta ya kiulimwengu ziko katika ardhi za Kiislamu, ima biladi za Kiarabu, Iran, barani Afrika, kama Nigeria au Asia ya Kati kama vile Kazakhstan, Turkmenistan au Caucasus, kama nchini Azerbaijan, lakini usafirishaji huo wa mafuta ng'ambo hauko mikononi mwa watu wake, ambao wengi wao wanateseka na umasikini na uchochole. Watawala, familia zao na wapambe wao wanayafuja na kuficha pesa ng'ambo. Pindi Amerika ilipoiomba Saudi Arabia mwaka jana wakati wa ziara ya Trump nchini Saudi Arabia mnamo 21/5/2017, kima cha dolari bilioni 460 familia ya Saud ilikuwa tayari kutekeleza matakwa yake na kulipa kiwango hicho. Hivyo basi, Waislamu hawataokoka na janga hili isipokuwa kupitia kwa Khalifa muongofu mithili ya Al-Farouq, Omar Ibn al-Khattab aliye gawanya utajiri kwa watu kwa usawa, na akaanza na masikini na kumalizia na Khalifa, ambaye ndiye wa mwisho kuchukua na kula. Mtume, mkweli (saw) amesema:

«كُلُّكُمْ رَاعٍ وَكُلُّكُمْ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ الْإِمَامُ رَاعٍ وَمَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ»

"Nyote ni wachungaji na nyote mutaulizwa juu ya mulivyo vichunga. Imam (mtawala) ni mchungaji na ataulizwa juu ya raia wake" [Bukhari]

Yeyote anaye wahadaa watu wake, adhabu yake ni kali kama alivyo sema Mtume (saw) katika Hadith iliyo simuliwa na At-Tabarani katika Al-Kabeer:

«مَا مِنْ عَبْدٍ يَسْتَرْعِيهِ اللَّهُ رَعِيَّةً، يَمُوتُ يَوْمَ يَمُوتُ غَاشّاً لِرَعِيَّتِهِ إِلا حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ»

"Hakuna mja yeyote anayetawalishwa na Allah kwa raia, akafa siku ya kufa kwake akiwa amewadanganya raia wake, isipokuwa Allah atamuharamishia Pepo juu yake." Hawa ndio watawala Ruwaibidha; wachache wa kufikiri na kudiriki!

**11 Safar Al-Khair 1440 H**
**20/10/2018 M**



Email: info@uqab.or.ke